SISI, WENGI WA WATENDAJI DUNIANI...

JINSI YA KUANDAA HAFLA NA MIKUTANO YA KITAIFA: MWONGOZO KUTOKA KWA WATENDAJI WA MITAA

Imewezeshwa na Movement for Community-Led Development, CIVICUS, na Peace Direct.

Yaliyomo

Utangulizi	**3**
Kabla ya Tukio: Watendaji wa Mitaa hubuni kwa pamoja Jedwali ambalo ni jumuishi, linaweza fikiwa na ni la kufaa	6
Wakati wa Tukio: Nafasi Salama, jumuishi na zinazoweza kufikiwa; Kwa washiriki wote	**10**
Baada ya Tukio: Maoni ya kukusudia na Ufuatiliaji	13
Hitimisho	**14**
Orodha ya waundaji wenza	**16**

Utangulizi

“Wapendwa Wafadhili na misingi ya nchi mbili na pande nyingi,,

Sisi, Mashirika ya kijamii na ya Mitaa kutoka kwa wengi duniani...”

Mnamo Novemba 2023, takriban watendaji elfu mbili wa wengi duniani waliandika barua kwa Wafadhili na waratibu wa Mikutano ya kimataifa kuhusu jinsi ya Kuandaa Nafasi na mazungumzo juu ya maendeleo yanayoongozwa na wenyeji. Barua hii ilizalishwa kutokana na ushirika wao, kufadhaika na kufedheha ya kutafuta ufikiaji wa meza ambayo inadaiwa iliundwa kwa ajili yao na bado kuwatenga. Barua hiyo iliweka kanuni tano zifuatazo kwa waratibu na Wafadhili ambao walijitolea kuitisha midahalo na Nafasi za kutekeleza maendeleo yanayoongozwa na wenyeji.

1. Hakikisha Watendaji wa Mitaa wapo mezani

Toka kwa wawakilishi wachache wa ishara wa dunia ya Wengi ili kuwa na uwakilishi sawa ya Mashirika ya Mitaa na Kijamii katika kufanya uwamuzi.

2. Hakikisha ufikiaji wa meza

Fanya Mikutano katika nchi ambapo Watendaji wa Wengi Duniani wanaweza kupata visa kwa urahisi zaidi.

3. Heshimu Ushiriki wetu

Toa notisi ya kutosha na ufadhili kamili, ikijumuisha visa, malazi, chakula/ marupurupu ya siku na gharama ya ada ya kuingia, mapema ili Mashirika ya Mitaa yaweze kushiriki.

4. Zungumza kwa lugha tunayoelewa

Kuwa na tafsiri ya Wakati mmoja, tumia lugha inayoweza kufikiwa katika nyenzo zote, na uwe na ufikiaji kwa watu wenye ulemavu ili watu kutoka katika mazingira tofauti waweze kushiriki.

5. Weka ajenda nasi

Unda ajenda na uwe mratibu pamoja na Mashirika ya Mitaa na kijamii na mitandao yao.

Barua hiyo ilipokelewa kwa uungwaji mkono mkubwa na kusababisha wito wa kupata Mwongozo zaidi kutoka kwa Watendaji walio wengi duniani kuhusu jinsi Mikutano hii inapaswa kupangwa. Kwa kuitikia wito huu, Shirika la Movement for Community-led Development (MCLD), CIVICUS na Peace Direct ilifanya kazi na watia saini wa barua asili ya walio wengi duniani ili kuunda hati ya Mwongozo. Dokezo hili la Mwongozo lilitokana na vipindi vya kusikiliza katika lugha nyingi na mazungumzo yaliyofanywa katika jukwaa la mtandaoni la lugha nyingi liitwalo Platform4Dialogue katika miezi ya Februari na Machi 2024. Watu 310 walishiriki katika vikao vya kusikiliza na mashauriano ya mtandaoni. Mbali na hatua hizi, uchunguzi ulitumwa kwa waandalizi na waandaaji wa midahalo na matukio ili kuelewa vikwazo walivyokabiliana navyo au wangeweza kukumbana navyo katika kubuni matukio ya maendeleo yanayoongozwa na wenyeji na Watendaji wa Mitaa, na Watendaji wa Mitaa kwa Watendaji wa Mitaa. Hati hii inanasa mafunzo kutoka kwa mashauriano haya kama mapendekezo ambayo Wafadhili na waratibu wote wanapaswa kuzingatia Wakati wa kupangwa matukio kwa ujumla, lakini hasa yale ya maendeleo yanayoongozwa na wenyeji. Haigemei tu juu ya vizuizi vinavyowakabili Watendaji wa Mitaa, lakini maono yao ya jinsi wangeandaa hafla kama hizo. Hati hii imeundwa kwa upamoja na Watendaji wa wengi duniani (tazama Orodha mwisho wa waraka) na inamilikiwa na kila mshiriki aliyehusishwa katika mchakato.

Miaka michache iliyopita imedhihirisha kwa uthabiti kwamba licha ya nia ya Wafadhili na Watendaji wengi kwenye uongozi kienyeji, kama inavyothibitishwa na Taarifa ya Wafadhili kuhusu Maendeleo yanayoongozwa na wenyeji na Ahadi ya Mabadiliko, kukosekana kwa usawa wa

madaraka kunaendelea kuwaweka kando Watendaji wa Mitaa katika mazungumzo juu yao. Watendaji wa Mitaa aghalabu huhisi kutosikilizwa na kutengwa katika mpangilio wa ajenda au mijadala katika mikusanyiko inayohusu ujanibishaji kwa sababu ya kutawaliwa na Watendaji na Wafadhili wa Kimataifa. Ili kuunda mazingira yanayofaa zaidi kwa ushiriki wa maana, makongamano yanapaswa kuelekezwa kwa ushirikiano wa kweli na Watendaji wa Mitaa. Hii ni pamoja na kuwashirikisha kikamilifu katika hatua za kupanga, kuhakikisha mawasiliano ya wazi kuhusu malengo ya kongamano, na kuweka kipau mbele mifumo thabiti ya kutoa maoni. Tunatambua kuwa mageuzi ya kimfumo ni safari, na nia yetu katika waraka huu ni kutumika kama washiriki wa Wafadhili na waratibu wanapotafuta njia ya kuongozwa kiwenyeji katika njia zao za kufikiri, kuwa na kufanya.

Mapendekezo ya lazima

Katika wito wa “hakuna chochote juu yetu, bila sisi,” Mikutano ya maendeleo inayoongozwa na wenyeji inapaswa kuongozwa na Watendaji wa walio wengi duniani kwa usaidizi na ufadhili kutoka kwa Watendaji wa wachache duniani/ Watendaji wa ulimwengu wa kaskazini. Hatahivyo, Tunatambua kuwa hili huenda lisiwezekane kila mara, hasa katika mfumo mbovu ambao unafanya kazi kwa sasa.
Hati hii ya Mwongozo inatoa mapendekezo ambayo tunazingatia mambo ya lazima. Yanaonyesha mabadiliko ambayo yanahitaji kufanywa maramoja ili kushughulikia kukosekana kwa usawa wa madaraka na kutoa hatua ambazo waratibu wote wanapaswa kuchukua ikiwa wana nia ya dhati juu ya maendeleo yanayoongozwa na wenyeji na wanakusudia kutekeleza kanuni tano zilizoainishwa na Watendaji wa wengi duniani katika barua yao.

Kwa urahisi wa matumizi, mapendekezo yameunganishwa katika vikundi vitatu: kabla ya tukio, Wakati wa Tukio na baada ya tukio.

Zaidi ya hayo, ingawa mapendekezo haya ya lazima ni hatua muhimu kuanzia ili kufanya mikutano iwe ya upamoja na wenye heshima, lakini haitoshi. Mapendekezo ya ziada ya kufanya mikusanyiko wenye Mwongozo wa kiwenyeji yametolewa katika visanduku vya samawati mwishoni mwa kila sehemu. Sisi, Watendaji wa wengi duniani, Tunatambua kuwa mabadiliko haiwezi kutokea maramoja. Mengi ya mabadiliko haya yanahitaji raslimali nyingi na huenda yasiwezekane mara moja. Pia Tunatambua kuwa kulingana na ukubwa wa mkusanyiko, madhumni na uharaka wake, sio mapendekezo haya yote yatahitajika au kuwezekana kila Wakati. Kwa hivyo tumeweka mapendekezo haya ya ziada Kama maswali ambayo waandaaji wanapaswa kuendelea kujiuliza, tukielewa kuwa majibu yanaweza kutofautiana kulingana na hali. Baada ya yote, muktadha ni muhimu.

Kabla ya Tukio: Watendaji wa Mitaa hubuni kwa upamoja Jedwali jumuishi, inayopatikana na inafaa kama

Ilivyoainishwa katika barua ya wengi ulumwenguni, maendeleo ya kweli yanayoongozwa na wenyeji ni juu ya kuhakikisha kuwa Watendaji mbalimbali wa walio wengi duniani hawapewi viti vichache tu katika meza, bali ni sehemu ya wanaobuni meza. Watendaji wengi duniani wanapaswa kuwa na jukumu kubwa katika uundaji wa dhana, kubuni na kutekeleza Mikutano ili kuhakikisha kuwa inahusisha na kukidhi mahitaji na vipaumbele vya Jamii za mashinani.

Masharti

Mtungo wa wakati, mahali, sababu na mtendewa

1. **Madhumuni na Ushiriki:** Kwa uwazi wasilisha kusudi, malengo na matokeo tarajiwa ya mkutano kwenye mwaliko/ tovuti/nyaraka zinazohusiana, katika lugha nyingi, pamoja na mchakato wa uwazi wa uteuzi wa wazungumzaji, vikao na washiriki waliofadhiliwa.

2. **Uwenyeji:** Daima zingatia kushirikiana na Shirika au mitandao ya Mitaa ili Kuandaa mkutano hata kama mkutano unafanyika ulimwenguni mwa wachache (Dunia ya Kaskazini).

3. **Muda:** Chagua tarehe angalau miezi 4-6 zijazo, na ikiwezekana, zaidi. Hakikisha washiriki wamethibitishwa angalau miezi 3 kabla tarehe ya mkutano ili kuwezesha. kupanga safari na visa. Kwa matukio ya kila mwaka, zingatia tarehe maalum(kila mwaka, kila # nambari ya mwaka) ili watu waweze kuyapangia mapema.

4. **Mahali:** Kwa matukio ya Kitaifa ya ana kwa ana, chagua nchi iliyo na vizuizi vidogo vya kuingilia, na ambayo haileti hatari kwa washiriki kulingana na usalama na utambulisho wao. Kumbuka, visa vinasalia kuwa mojawapo ya vikwazo vikubwa kwa washiriki wa wengi duniani. Pima ubora wa mashauriano ya mtandaoni na ya mseto dhidi ya ana kwa ana. Vilevile, fikiria mikutano ya kikanda. Hizi hutoa ufikiaji mkubwa kwa Watendaji wengi duniani na pia hupunguza mkanyago wao kikaboni.

Hakikisha ufikiaji wa meza

1. **Usajili:** Eleza kwa uwazi vigezo vya uteuzi wa ushiriki, gharama, na kile kitakachotolewa chini ya usaidizi wa kifedha. Maswali ya maombi hayapaswi kuchukua muda mwingi – kwa hakika, yanapaswa kuchukua si zaidi ya dakika 60 kujaza. Kutoa fomu ya maombi iliyorahisishwa na rahisi kutumia, na chaguo la kuhifadhi ukiendelea na kuikamilisha katika hatua nyingi pia inasaidia.

2. **Ufikiaji mpana na wa kusudi:** Mawasiliano yote yanapaswa kuwa katika lugha nyingi, kupitia hati rahisi, na katika njia pana ya mawasiliano ikijumuisha tovuti, majukuaa ya mitandao ya kijamii, na mitandao/ Mashirika asasi ya kiraia. Ufikiaji wa lugha unaweza kuwa ghali, lakini, kwa uchache hakikisha nyenzo katika lugha rasmi za Umoja wa Mataifa na lugha kuu ya eneo ambalo tukio linafanyika, hasa ikiwa ni katika ulimwengu mwa wengi. Tafuta kwa bidi sauti ambazo haziskiki kuakisi lenzi ya mkutano. Wanawake kutoka dunia ya wengi, walio wachache, walemavu, wazee, vijana na watu wa kiasili kutoka nchi mbalimbali hulete mtazamo mbalimbali. Alika anuwai

ya vikundi, hasa wale walio nje ya miji kuu, kuwasilisha wito makaratasini au ata kushiriki kwenye paneli, na uwazi kwa mchakato na uteuzi. Na tamati, kumbuka kuwa maswali kuhusu uzoefu yanaweza kuwa vikwazo kwa vijana.

3. **Taratibu za uchaguzi:** Alika Watendaji wa Mitaa kutoka dunia ya wengi kuwa sehemu ya kamati ya uteuzi ili kuhakikisha utofauti katika sauti. Alika mitandao ya wengi duniani kutambua/kuchagua wazungumzaji kutoka kwa miktadha yao badala ya washiriki kutoka kwa dunia ya wachache kuwaalika wale ambao tayari wanawajua.

4. **Msaada wa kifedha:** Lipia ada zote au nyingi ya ada za usajili katika mkutano, nauli ya ndege, ada za visa,malazi, mlo, matukio, SIM kadi au mawasiliano na bima kwa Watendaji wengi wa dunia. Lipia gharama ya kusafiri kutoka na kuenda kwa uwanja wa ndege,kulingana na ratiba za ndege, kwani baadhi ya Watendaji wengi duniani hulazimika kusafiri masafa marefu ili kufika uwanja wa ndege wa kitaifa. Lipieni washiriki malazi na nauli ya ndege kwanza kuliko wajilipie nanyi muwarudishie, gharama kama hizi za mwanzo huweza kuwa tatanishi. Tambua kuwa gharama za visa huongezeka zaidi ya ada za visa, na ni pamoja na kusafiri kwa balozi (Katika nchi za utatu wakati mwingine), posta na picha, nk. Eleza kwa uwazi ni gharama yepi yatalipiwa na yepi hayatalipiwa (k.m. kama visa imekataliwa, ada za kukatiza visa, ndege na hoteli yatarejeshwa?), ili kuwezesha washiriki wengi duniani kufanya uamuzi sahihi kuhusu ushiriki. Jumuisha gharama ya kuandamana na mlemavu, kama inahitajika.

Mambo ya kufanya 1: Je, tunawezaje kubuni matukio ya mtandaoni na ya kimseto jumuishi na yenye uwezo wa kufikiwa?

- Hakikisha usawa kwa Wakati kwa Watendaji wengi wa duniani. Wasilisha saa na Wakati kwa utofauti wake kulingana na eneo. Gawanya tukio kwa siku tofauti tofauti. Epuka Ijumaa, ni siku kuu kwa nchi mingi.
- Zingatia ukubwa wa kipindi na mifumo ambayo sio nzito kwa utumiaji wa data na rahisi kuelekeza. Chagua jukwaa shirikishi na utoe mwongozo wa hatua kwa hatua ya jinsi ya kupitia na inapowezekana toa vipindi vya mazoezi (na jinsi ya kuingia kwa kuwa zana nyingi zinahitaji unununzi).
- Hakikisha mwongozo uliopo ni wa kompyuta na rununu, hasa vifaa vya android na katika lugha nyingi.
- Zingatia kurejesha pesa ya mtandao na wa data.
- Hakikisha nyenzo zote za mikutano zinashirikishwa mapema na katika lugha nyingi.
- Ukiwauliza washiriki kuwasilisha maswali mapema, hakikisha maswali hayo yanashughulikiwa wakati wa tukio.
- Unda nafasi za mitandao kwenye jukwaa ya lugha nyingi au jijumuishe katika vikundi vya LinkedIn na WhatsApp vinavyowezesha washiriki walio mbali kungamana na matukio ya ana kwa ana.
- Tuma rekodi kwa barua pepe kwa washiriki waliojiandikisha ambao hawakuweza kuhudhuria kwa sababu za kifundi, changamoto za kieneo na kiwakati au vikwazo vya umaskini.

Mbali na haya, kwa matukio ya mseto:

- Hakikisha usawa kwenye vikao (sio eti Watendaji wengi wa dunia ya wengi wako mtandaoni na walio wachache/ Ulimwengu wa Kaskazini wamehudhuria ana kwa ana). Ambapo bajeti ni ndogo, fikiria kufadhili washiriki wapya kutoka dunia ya wengi ili waweze kuhudhuria vikao vya ana kwa ana na kuhimiza washiriki waliotangulia kujiunga mtandaoni.
- Hakikisha kuwa muundo wa tukio haufanyi washiriki kutoka mbali kujihisi kama washiriki wa kujaza tu; kwa kusudi wahusishe kwa ajenda.
- Zingatia ufikiaji wa Lugha na tafsiri kati ya tukio ya ana kwa ana na kwa mtandao.

5. **Usaidizi wa kujiandaa:** Toa maagizo ya kina ya jinsi ya kujiandaa, jinsi ya kusafiri na jinsi ya kushiriki. Weka dawati la usaidizi ili kusaidia washiriki katika mchakato wa kutuma ombi ya visa, lipia safari ya ndege kwa kushauriana na Watendaji wa Mitaa (kwa kuzingatia hitaji ya visa vya usafiri, na kupunguza hatua za visa kwa Watendaji wa Mitaa), na saidia katika uhifadhi wa malazi. Toa mwongozo wa habari juu ya mchakato wa uamiaji toka nchi moja hadi nyingine, usaidizi katika uwanja wa ndege na itifaki, na usafiri wa ndani, pamoja na hali ya hewa na mavazi yanayofaa, na kuzingatia chakula, nk. Tambua kuwa hatua hizi zinaweza kuwa geni na zisizofaa kwa baadhi ya washiriki na kurahisisha utaratibu ni muhimu kwa wahusika kuhisi kukaribishwa na kuwepo. Mkutano au video ya muhtasari wa kabla ya kuwasili ili kuangazia maelezo haya inaweza kusaidia.

Kuweka Ajenda na watendaji wengi duniani

1. Tanguliza utofauti katika kamati ya mipango ili kuhakikisha ushiriki kutoka mikoa mbalimbali na mitazamo. Na hakikisha Watendaji wa dunia ya wengi wanaohusika katika kupanga wanalipwa fidia kama ishara ya heshima kwa maarifa na wakati wao. Hii itahakikisha kwamba kamati ya mipango itakuwa na uelewaji mzuri wa aina ya stadi zinazohitajika, ikiwa ni pamoja na fedha na usafiri.

2. Tumia mchakato wa mashauriano kuweka na kumiliki ajenda, tengeneza nafasi ambazo zimezingatia usawa , na kutambua wazungumzaji na Watendaji wa Mitaa. Hili linaweza kufanywa kwa njia bunifu na shirikishi ikijumuisha uchunguzi na mashauriano ya kabla tukio, kupata mitandao ya kiwenyeji na kuunda vikundi vya asasi za kiraia mapema ili kuratibu upangaji.

Mambo ya kufanya 2: Ni hatua gani zingine tunaweza kuchukua ili kufanya Mikutano ya ana kwa ana kufikiwa zaidi?

- Amua ikiwa mkutano wa kimataifa, wa kikanda au ya mitaa inahitajika. Kuitisha hafla katika ngazi za kikanda na mitaa zina uwezekano mkubwa wa kuhimiza ushiriki wa Watendaji wengi duniani. Kupanga matukio kulingana na eneo kunaweza pia kupunguza gharama na alama ya kaboni. Ikiwa unapanga tukio la Kitaifa, chagua nchi ya amani na usalama (hasa kwa wanaharakati wanaokandamizwa kulingana na maoni yao) na pale ambapo vizuizi vya kuingia viko chini, kama vile Mauritius.

- Kwa matukio ya mara kwa mara (km. kila mwaka), fikiria kuyaweka kwa nchi yenye uchama kwa msingi wa mzunguko, ukiyapa vipaumbele nchi yenye vikwazo vidogo katika usafiri.

- Toa usafiri wa kuenda na kutoka uwanja wa ndege na mahali pa mkutano/hoteli, hasa kwa wajumbe wanaofika usiku sana au mapema asubuhi. Mifumo ya usafiri ni tofauti katika nchi tofauti na si kila mtu anajua jinsi ya kuielekeza au ana kadi za mkopo/fedha za kulipia tikiti.

- EHakikisha maelezo ya kina kuhusu michakato ya visa, ili kuwawezesha washiriki kuelewa wakati na uwezekano wa kupata visa. Toa vituo vya mawasiliano vinavyopatikana kwa urahisi kwa maswali yoyote washiriki wanaweza kuwa nayo. Ikiwezekana, na pale ambapo chaguo zipo, wasaidie washiriki kupata visa vingi vya kuingia, hasa kwa majimbo ya Schengen.

- Hakikisha malazi, kama vile vituo vya kulelea watoto kwa wazazi, inaonyesha kujitolea, ujumuishi na heshima kwa mahitaji na mapendeleo mbalimbali.

- Tambua maeneo tofauti ambayo yangezungumziwa vyema na walioathirika moja kwa moja. Tambua ingawa wanawakilisha jamii iliyotengwa, Watendaji wengi wa dunia pia ni watu binafsi walio na uzoefu wao wenyewe na hawapaswi kuhisi shinikizo la kuzungumza kwa niaba ya jamii yao. Wafikie kabla tukio ili kuona majukumu ambayo wangependa kucheza na maeneo ya kushiriki.

- Fikia mashirika yanayofanya kazi na watu walioathiriwa au waliotengwa na uombe miunganishi au uteuzi ya watu binafsi.

- Himiza usawa wa kijinsia katika ushiriki.

- Hakikisha ukumbi unapatikana (rahisi kupata, njia panda na/au ufikiaji wa lifti/ rahisi kufikia).

Mambo ya kufanya 3: Ni hatua gani za ziada tunahitaji kuchukua mapema ili kuhakikisha afya, usalama na ustawi wa washiriki katika mikutano ya ana kwa ana?

- Shiriki maelezo ya chanjo mapema iwezekanavyo ili washiriki wapate muda wa kutafuta mahitaji ya matibabu. Eleza mpango wa afya na usalama wa washiriki ikijumuisha mipango ya waandaaji kulipia gharama za ziara za hospitali. Kulingana na muktadha, shiriki jinsi waandaaji wamehakikisha mazingira salama kwa washiriki, ikijumuisha itifaki za COVID-19 na mipango ya usafiri wa ndani.

- Unda nafasi za kupumzika, ustawi na usaidizi wa kirika ili kutambua dhiki inayoweza kutokea na kulemea washiriki, hasa wale wanaohudhuria makongamano kwa mara ya kwanza au kutoka kwa mazingira yenye changamoto. Kwa mfano, mkutano wa The Shift The Power ya Bogotá 2023 ilikuwa na pahali pa kusinzia na machela mazuri; mkutano wa Women Deliver ya Rwanda 2023 ilikuwa na chumba tulivu, sehemu ya maombi na mshauri. Tafakari dawati la usaidizi ya marika na dawati la dharura la matibabu. Hakikisha kuwa washiriki wanajua kuwa sio lazima kuhudhuria kila tukio na jopo.

Kuheshimu Ushiriki Wetu: Kusudi kwa Kushirikishwa na Ushiriki Hai

1. **Mienendo ya Madaraka:** Jumuisha njia za kuzuia kutengwa kimtazamo na Watendaji wa wengi duniani katika kila hatua ya tukio. Fikiria mienendo ya madaraka isiyo wazi. Ofisi za nchini za Mashirika yasiyo ya kiserikali haziwezi na hazifai kuchukua nafasi ya Mashirika ya Mitaa au ya Kitaifa na pia wajumbe wanaofadhiliwa na serikali kutoka dunia ya wengi. Tetea kutambuliwa, uhalali na nafasi kwa Mashirika ya Mitaa /Asasi za kiraia /Mashirika mashinani.

2. **Usikivu wa Kitamaduni:** Usaidizi/Muunganisho wa kitamaduni ni muhimu kwa ajili ya kuunda mazingira yenye mkutano ya kujumuisha na ya heshima, hasa kwa washiriki wanaotoka kwenye mikoa yenye migogoro inayoendelea au asili mbalimbali za kitamaduni. Baadhi ya washiriki kutoka ulimwenguni mwa wengi wanaweza kuwa wanasafiri nje ya nchi yao kwa mara ya kwanza na wanaweza kupata mshtuko wa kitamaduni. Waandalizi wanapaswa kukabiliana na mambo haya kwa tahadhari na kuelewana kwa washiriki kutoka kwa Mashirika yenye vikwazo au maeneo yaliyoathiriwa na migogoro. Wanapaswa kujumuisha maelezo kuhusu kanuni za mavazi katika nyenzo za muhtasari ili kuhakikisha kuwa washiriki wanaelewa kuwa wanakaribishwa kuvaa mavazi rasmi au ya kawaida (jinsi itakavyokuwa) kutoka kwa tamaduni zao. Nyenzo fupi pia zinafaa kutoa habari kuhusu hali ya hewa na kubainisha kama ukumbi utakuwa na kiyoyozi au joto ili washiriki wajiandae sawasawa. Wajumbe wengi wa mara ya kwanza hawana uhakika ya nini cha kutarajia katika Mikutano ya kitaifa.

3. **Kujenga Miunganisho:** Itakuwa bora kutilia maanani mikutano ya kabla ya tukio.Hili litasaidia kuwezesha miunganisho na uaminifu mapema.

4. **Utunzaji na ustawi:** Uchovu wa ndege na safari za mbali ni tata, haswa kwa wasafiri wa mara ya kwanza. Pale ambapo bajeti inaruhusu itakuwa bora kuzingatia usiku wa ziada kabla ya mkutano ili washiriki wapate mda wa mapumziko. Hili litawasaidia kushiriki katika matukio kikamilifu. Kwa washiriki wanao safiri toka maeneo ya mizozo (k.m Palestina, Demokrasia ya Kongo, Ukraine) washughulikiwe kupata mipango ya dharura iwapo hawatoweza kusafiri kurudi nchi au jiji lao kutokana na ongezeko la migogoro au utata katika mipaka, na kadhalika.Hakikisha kwamba wanatengewa fedha za kugharamia makaazi marefu yasiyotarajiwa.

5. **Ujumuisho wa Kukusudiwa:** Ni muhimu kuzingatia ufikiaji wa vyumba vya kibinafsi kwa Watu Wenye Ulemavu na washiriki wa LGBTQI+. Inapowezekana, ni bora kuwahamasisha wafanyakazi wa ndani, hasa wakati wa kufanya matukio katika nafasi au nchi ambazo zinazidi kuweka vikwazo kwa jumuiya za LGBTQI+.

Wakati wa Tukio: Nafasi salama, jumuishi na zinazoweza kufikiwa kwa washiriki wote

Masharti ya kufanywa

Kuhakikisha upatikanaji wakati wa tukio

1. **Lugha:** Hakikisha kuna utafsiri katika lugha nyingi, nukuu ya wakati halisi (kwa matukio ya mitandao) na tafsiri ya lugha ya ishara. Tafuta njia za kusaidia watu kujiskia vizuri na tafsiri, badala ya kuhisi kulazimishwa au kushinikizwa kutumika lugha ya mkutano. Watie moyo watu kuzungumza kwa lugha yao ya asili zaidi ya tafsiri, k.m. kwa kuuliza kila mmoja kusalimiana au kusema kwaheri kwa lugha yake, kuruhusu mwelekezi kuzungumza kwa lugha yao ya asili, kuwa na vipindi tofauti na lugha tofauti za msingi (na tafsiri). Kwa lugha ya msingi zingatia lugha inayozungumzwa na washiriki wengi, iwe ni lugha asili ya waandaaji au la.

2. **Nyenzo:** Nyenzo kabla, wakati na baada ya mkutano pia zinapaswa kutafsiriwa na kushirikiwa mapema ili kusaidia watu kufahamu istilahi, wakiwemo watafsiri wenyewe. Epuka nyenzo za kiufundi na vifupisho katika nyenzo za mikutano – kumbuka wengi watakuwa wakisoma haya katika lugha ambayo sio lugha ya kwanza au pili.

3. **Ufikivu:** Hatua za ufikiaji ni ikiwa pamoja na malazi ya walemavu, manukuu ya wakati halisi, na ukalimani wa kimataifa wa lugha ya ishara unahitaji kuwepo, si tu kwa mkutano mkuu bali kwa vikao vyote. Mipango ya usafiri na malazi pia inafaa kuzingatia uhamaji na changamoto za ufikiaji.

Kubuni maeneo salama na jumuishi

1. **Maeneo salama:** BJenga nafasi ambazo ni salama kushiriki bila kujidhibiti. Hii inaweza kuhitaji nafasi bila wafadhili au wawakilishi wa serikali (na usomaji kwao baada ya ukweli). Zingatia hatari ambazo baadhi ya watetezi na wanaharakati wanaweza kukabiliana nazo wanapozungumza kwa uaminifu. Wanaharakati, ambao wana wasiwasi wa usalama na hitaji ya kutojulikana, wanahitaji kulindwa kwenye hafla ili waendelee kwa usalama kazi zao muhimu. Fikiria kuongeza vitambulisho au vibandiko kwa washiriki wasiotaka picha au kurekodiwa. Soma kanuni za maadili au seti ya viwango kabla ya mkutano kuanzaa (k.m. kutovumilia unyanyasaji, nk.)

2. **Kukabiliana na Dhiki:** Saidia afya ya akili na ustawi ya washiriki kupitia nafasi za kupumzika, shughuli za akili na raslimali za afya ya akili ili kusaidia washiriki kudhibiti mafadhaiko au uchovu wowote wanaoweza kupata wakati wa tukio.

3. **Himiza Miunganisho:** Kuunda mitandao, kuongeza mwonekano na kujenga mshikamano ni baadhi ya sababu kuu kwa Watendaji wengi duniani kushiriki katika Mikutano ya kitaifa. Kwa hivyo, waandaaji wanapaswa kuwezesha fursa za kutangama nje ya paneli ambazo zinasaidia watu ambao labda hawajui wengine kwenye mkutano ili kuzungumza na kufahamiana (sio tu kwa mapumziko ya kahawa au masaa ya furaha)

4. **Muundo wa Kikao:** Hamisha mwelekeo kutoka kwa wazungumzaji waliochaguliwa na ujenge muda zaidi wa kujifunza na kutafakari kati ya washiriki.

5. **Uwezeshaji Jumuishi:** Wawezeshaji wanapaswa kuhimiza mitazamo mbalimbali na kusikiliza kikamilifu, ili kuhakikisha washiriki wanahisi kuthaminiwa na kuheshimiwa. Ni lazima watoe muda kwa washiriki kujiongelea na kuruhusu wengine kutafakari na kuitikia, ili washiriki waweze kujifunza kwa na kila mmoja. Hii inafanywa vyema katika vikundi vidogo, ambapo uwezeshaji mzuri hukuza mazingira magumu na huruma na hujenga mahusiano. Fikiria kuwa na Watendaji wa dunia ya wengi katika hafla moja na wale kutoka ulimwengu mwa wachache/Dunia ya Kaskazini.

Mambo ya kufanya 4: Tunawezaje kuhakikisha ushiriki wa maana ya Watendaji wengi duniani Wakati wa hafla za ana kwa ana?

- Nyaraka zote zinazohusika, ikijumuisha ajenda na ratiba ya mkutano, dhana, majukumu na matarajio ya wawakilishi, fursa za kuzungumza na kuandaa vikao, hisia ya nani mwingine amealikwa, kile kinahitajika kuhudhuria (ikiwemo raslimali), na barua ya mwaliko inapaswa kutolewa mapema (miezi 3 ni sawa) ili kuwawezesha Watendaji wengi duniani kuamua kama wanafaa kuhudhuria mkutano na kupanga safari zao.

- Hati muhimu za mikutano kama vile dhana, ajenda na ratiba zinapaswa kutafsiriwa katika lugha rasmi za Umoja wa Mataifa kwa uchache na kushirikiwa mapema zaidi. Kama wawakilishi wa Jamii pana, hii pia inaruhusu muda kwa washiriki kupata michango kutoka kwa Jamii, wafanyikazi wenzao nk. Ili waweze kusaidia kuwasilisha mawazo yao.

- Zingatia ufikiaji zaidi ya lugha za Umoja wa Mataifa- k.m. Kiswahili au Kiingereza Pijini au Kiewe kulingana na mahali mkutano unaandaliwa. Jaribu kutumia waakalimani wa Mitaa; Hakikisha wakalimani wana uwezo wa kujifahamisha mada na misamiati muhimu kabla. Hakikisha tafsiri ya wakati mmoja haipatikani tu katika kikao cha jumla bali pia katika vyumba vya vipindi vifupi.

- Kumbuka kwamba ishara na mkao wa uso humaanisha vitu tofauti katika lugha/tamaduni tofauti.

- Anzisha na usambaze miongozo iliyo wazi ya mawasiliano ya heshima, ambayo inahimiza mitazamo mbalimbali, hutoa fursa kwa washiriki wote kushiriki utaalamu wao na kuhakikisha michango yote inakubaliwa na kutathminiwa.

- Nafasi zinazopunguza idadi ya washiriki wa Mashirika ya Kitaifa na Serikali,husaidia kuweka kipaumbele sauti na mitazamo ya Mashirika ya Mitaa na mashinani.

- Kwa makusudi,unda nafasi za kuonyesha kazi za Mashirika ya Mitaa na kushiriki hadithi za mafanikio. Unda nafasi mbadala ya kushiriki, ikiwa ni pamoja na kuwasilisha nyenzo mapema, kama barua, maombi, podkasti au video, kwa washiriki ambao hawawezi kupata jukumu la kuzungumza.

- Wezesha nafasi za kuunganisha zinazoingiliana (ikijumuisha kwa uwazi katika nchi na tamaduni zote, na kwa njia zinazounga mkono watu wasiojuana au wanaowajua wengine kwenye mkutano kuungana) badala ya kutanguliza tu vikao vya mashauriano.

- Jenga aina zaidi ya mikutano midogo (kama mazungumzo kando ya moto, warsha) katika ajenda ya kuhudumia mitindo mbalimbali ya kujifunza na aina za kujenga uhusiano. Inajumuisha nafasi za kujenga ujuzi laini, ushirikiano, mazungumzo na wafadhili, shughuli zinazoziba pengo kati ya aina tofauti za mashirika na mashirika kutoka mikoa tofauti. Ondoka kutoka kwa mihadhara ya kitamaduni na paneli.

- Toa nafasi kwa washiriki kujieleza kwa njia mbadala, kama vile kuandika, kuchora, au mawasilisho ya kisanii, ili kuhakikisha ushirikishwaji zaidi, hasa kutoka kwa watu ambao hawawezi kujiamini sana au kustareheshwa na kuzungumza mbele ya watu.

- Kuwa na msimamizi dhabiti ni ufunguo wa kubadilisha mienendo ya madaraka.

- Miingiliano ya kitamaduni kama vile ngoma za kitamaduni na muziki kutoka kwa nchi ya washiriki huwafanya washiriki kuhisi wameunganishwa na kustareheshwa zaidi. Wakati makongamano yanapofanyika katika dunia ya wengi, zingatia kujumuisha kutembelea Jamii au Mashirika ya Mitaa ambayo yanaunga mkono kazi inayoongozwa na jamii.

- Unda nafasi za mazungumzo kati ya vizazi na kubadilishana maarifa ili kuhakikisha kwamba mahitaji ya kujifunza ya wajumbe inatimizwa. Fikiria kuanzishwa kwa programu za ushauri ambapo Watendaji wenye uzoefu wa dunia ya wengi wanaweza kuwaongoza wanaohudhuria mkutano kwa mara ya kwanza na kuunda fursa kwa vijana.

11

Mambo ya kufanya 4 (Inaendelea): Tunawezaje kuhakikisha ushiriki wa maana wa Watendaji wengi duniani wakati wa hafla za ana kwa ana?

- Mpangilio wa nafasi na vyumba ni muhimu ili kuunda mazingira ya kukaribisha na kujumuisha. Zingatia ufikiaji wa umbizo na ujumuishaji wa nafasi hasa kwa watu wenye ulemavu.
- Chache ni zaidi- Mara nyingi makongamano hujaa na yanaenda kasi sana. Punguza kiasi cha maudhui yaliyoratibiwa na yasiyobadilika ili kuruhusu nafasi ya uigaji, kushirikiana na ustawi.
- Anzisha ukaguzi wa mara kwa mara na njia mingi za washiriki kushiriki mahangaiko au kuuliza maswali bila kuhisi kudunishwa au kutengwa.
- Jenga nafasi mwishoni/ siku ya mwisho ili kupata suluhisho na ahadi na uhakikishe malengo ya mkutano yamefikiwa. Ikiwa hazijafikiwa, tambua nia hatua gani zinazofuata kwa Wakati huu.
- Hakikisha usikivu kwa mazoea ya kitamaduni na kidini, hasa kwa washiriki kutoka asili tofauti. Hii inaweza kuhusisha kutoa nafasi za maombi, kushughulikia vizuizi vya lishe na kuhakikisha vituo vya chakula vimetiwa alama wazi. (k.m. mboga, halali), na kuheshimu taratibu za kidini kama vile Ramadhani. Kwa mfano, mkutano wa WomenLift Health Tanzania mwaka wa 2024 ilifanikisha iftari kwa wawakilishi wote kama ilivyokuwa katika mwezi wa Ramadhani.
- Kwa Uwajibikaji na Uwazi, Ufuatiliaji na washiriki wote ili kubadilishana maendeleo tangu mkutano, ikiwa ni pamoja na jinsi na kama malengo yalifikiwa. Rekodi mijadala na uwezeshe Ufuatiliaji wa ratiba ilito wazi na mipango ya utekelezaji.
- Kuanzisha vikundi vya kuzingatia Wakati wa tukio la ushirikiano unaoendelea husaidia kudumisha kasi na uwajibikaji zaidi ya mkutano wenyewe.
- Kuwezesha ushirikiano na kubadilishana maarifa kati ya makongamano ya Mitaa katika mikoa mbalimbali ili kuinua matokeo yao ya pamoja.
- Taja kwa Uwazi viashirio muhimu vya utendaji vya tukio na ushiriki maelezo haya na washiriki wote ili kuonyesha kujitolea kwa ujumuishi. Viashirio hivi vinaweza kujumuisha idadi ya washiriki kutoka kwa dunia ya wengi, kiwango cha ushiriki wao,utofauti ya mitazamo inayowakilishwa,na matokeo yanayoonekana kupatikana kupitia mkutano huo.

BAADA

Baada ya Tukio: Maoni na Ufuatiliaji wa kusudi

Masharti ya kufanywa

Watendaji wa Mitaa kwenye meza: Nini kinafuata

1. **Uwazi juu ya Mchakato:** Kutoa mawasiliano ya wazi mwanzoni kuhusu jinsi Taarifa inayotokana na tukio itatumika na hatua za Ufuatiliaji ni muhimu kwa kujenga uaminifu na uajibikaji.

2. **Taratibu za Ufuatiliaji:** Kutengeneza mifumo ya Ufuatiliaji kama vile ripoti za baada ya mkutano, upatikanaji wa vipindi vilivyo rekodiwa, majukwaa ya mtandaoni ambayo washiriki wanaweza kujihusisha nayo baada ya kongamano kumalizika, kugawana raslimali/ripoti, na inapowezekana na inavyotakikana na washiriki, nafasi ya kujijumuisha kwa ajili ya kuendelea kushirikiana inahakikisha kwamba washiriki wanapata fursa endelevu ya kukaa na habari na kuhusishwa.

3. **Kufunga kitanzi cha maoni:** Kufunga kitanzi cha maoni kwa kuhimiza na kushiriki maoni kutoka kwa washiriki, pamoja na kuwajulisha kuhusu hatua zozote zilizochukuliwa kutokana na maoni hayo, kunakuza Uwazi na kunaonyesha dhamira ya kuendelea kuboresha.

Hitimisho

Hati hii ni mkusanyo wa mwongozo kutoka kwa Watendaji walio wengi duniani kuhusu jinsi ya kushughulikia ukosefu wa usawa ya madaraka katika matukio. Inahitaji ushirikishwaji, ubia sawa na uwazi. Tunatambua kwamba maeneo mbalimbali ya mikutano yana malengo tofauti na mara nyingi yanahitaji kupangwa kulingana na hayo. Pia tunatambua kuwa kimo na raslimali zinazopatikana zina jukumu kubwa katika uundaji wa nafasi za kukusanyika. Miongozo hii imeundwa ili kuwawezesha waitifaki kufikiria kwa kina kuhusu kanuni na maadili ambayo yanasimamia nafasi wanazowezesha. Kuhama kutoka kufikiria juu ya hafla na mikutano kama mikusanyiko moja kwenda kwa nafasi za maksudi zinazounda muunganisho na hatua ya pamoja na kutuwezesha kupinga ukosefu wa usawa wa madaraka ulioenea katika mfumo wetu.

Sisi, Watendaji wengi duniani, tunakaribisha majadiliano yanayoendelea kuhusu mapendekezo haya tunapofanya kazi pamoja ili kutekeleza mapendekezo yalioainishwa katika barua yetu.

WAKATI WA BAADA

HAKIKISHA WATENDAJI WA MITAA WAKO MEZANI

HAKIKISHA TUNAWEZA KUFIKIA MEZA

HESHIMU KUSHIRIKI KWETU

ONGEA KWA LUGHA TUNAYOELEWA

WEKA AJENDA NASI

ORODHA YA WAUNDAJI -WENZA

Mamia ya waundaji-wenza walihusika katika uundaji wa hati hii. Orodha kamili ya majina inapatikana kwa.

1. Aalem for Orphan and Vulnerable Children, Inc. – Liberia
2. Abdourahamane Diallo – Guinea
3. Aben Melvis Anep – Cameroon
4. Abera Yenework Kebede (PhD) – Ethiopian
5. Abundant Favour Christian Ministries International – Uganda
6. Acción por los Niños – Perú
7. Accountability Lab Nigeria – Nigeria
8. Action Contre la Pauvreté, ACP – Burundi
9. Action for Humanity & Social Progress – Bangladesh
10. Action Pour la Promotion des Vertus au Congo – Democratic Republic of the Congo
11. Actions Contre les Souffrances des Orphelines et Veuves – Democratic Republic of the Congo
12. Adamson Nsimba – Tanzania
13. ADDHF-DUKUNDANE – Burundi
14. Adem Asociación Por Los Derechos De Las Mujeres Co Fundadora De La Campaña Nacional Por El Derecho Al Aborto Legal Seguro Y Gratuito – Argentina
15. Adinani Mussa – Tanzania
16. Advocate For Social Justice and Development Sierra Leone – Sierra Leone
17. Aero Integrated Development (AID) – Uganda
18. AFeJE ONG – Benin
19. Afghan Youth Forum for Democratic Affairs – Afghanistan
20. Afiavi SEHONOU – Benin
21. African Children and Youth Development Network (ACYDN) – France
22. Agath KOUNNOU – Benin
23. Ahmed ALLOUCH – Tunisia
24. Ajuadem Nixon Atem F
25. Al-Ghad Foundation for Investment in Human – Iraq
26. Alex Kiptorus
27. Alex Martins
28. Aliyu Barau Yola, Sahawa Youth Development Organization – Nigeria
29. Alma Cívica – Paraguay
30. Aloro Gordon Paul – Uganda
31. Alpha Action for Social and Economic Development (AASED) – Uganda
32. Amazon Theatrix Ensemble – Kenya
33. Ammaarah Nilafdeen – Sri Lanka
34. Andrea Vignolo
35. Angella Atayo – Uganda
36. Anima Sharma – India
37. Annesha Kar Gupta
38. Appui Solidarité Pour le Renforcement – Mali
39. Asli Telli – Turkey & Germany
40. Asociación Juvenil Indígena de la Moskitia - AJIM – Nicaragua

ORODHA YA WAUNDAJI -WENZA

41. Asociación Nacional De Deporte Anade LGBTQ+ – Mexico
42. Asociación Unión de Talleres 11 de septiembre – Bolivia
43. Association Burkinabé de Fundraising – Burkina Faso
44. Association des Femmes Vulnérables Aveugles et Malvoyantes (AFVAM) – Congo-Brazzaville
45. Association Djazairouna des Familles Victimes du Terrorisme Islamiste (Membre observateur de la Commission Africaine des Droits de l'Homme et des Peuples) – Algeria
46. Association for Farmers Rights Defense (AFRD) – Georgia
47. Association For Promotion Sustainable Development – India
48. Ayabavi Linda Ophélie COMLAN SESSI
49. Bate Tabenyang Alaine – Cameroon
50. Berns Komba Lebbie (Land for Life, Sierra Leone) – Sierra Leone
51. Birkti Nigussie
52. BOAD, Bureau Oecumenique d'Appui au Developpement – Democratic Republic of the Congo
53. Break Margins Africa – Kenya
54. Brothers Keeper Organisation – South Africa
55. Build Peace and Development – Democratic Republic of the Congo
56. Bukedi Civil Society Organisations' Network – Uganda
57. Camkwoki Grassroot Initiative For Development Limited – Uganda
58. Catherine Bartenge
59. CEAMUJER Nicaragua – Nicaragua
60. CEDEAL – Ecuador
61. Celine Osukwu
62. Centre for Faith and Community Development – Nigeria
63. Centre for Peace and Development (CPD) – South Sudan
64. Centre for Peace and Secular Studies – Pakistan
65. Chris O. Owalla – Kenya
66. Christelle ASSOGBA – Benin
67. Christian Elongue – Cameroon
68. Christopher Chirambo
69. Ciara Watson
70. CIDDH-RDC – Democratic Republic of the Congo
71. Cihan Koral – Turkey
72. Civil Society Advocacy Network on Climate Change and the Environment Sierra Leone (CAN-SL) – Sierra Leone
73. Claire Nelson
74. Claude Marie Bernard Kayitare – South Africa
75. Coalition Action For Preventive Mental Health – Kenya
76. Coalition des Volontaires pour la Paix et le Développement (CVPD) – Democratic Republic of the Congo
77. Coalition of Somali Human Rights Defenders CSHRDS – Somalia

ORODHA YA WAUNDAJI -WENZA

78. Community Based Organisations Coalition for Human Rights and Good Governance – Malawi
79. Community Food Security - ASAC Togo – Togo
80. Community Initiative Action Group – Kenya
81. Conseil Territorial de la Jeunesse de Rutshuru – Democratic Republic of the Congo
82. Consolata Soyiri Dassah – Ghana
83. Constance MUKARATI
84. COOJED Ltd – Rwanda
85. Corporación Cambio Sostenible – Colombia
86. CSO Network - Kisumu – Kenya
87. CSYM HUDUMA – Tanzania
88. Dandjiman Kabirou Adjara – Benin
89. Daniel Enock Manoba – Ghana
90. Davis Okeyo
91. DEDRAS ONG – Benin
92. Dr. Sokfa John – South Africa
93. Dream Centre for Young Minds – Nigeria
94. EDDIB Burundi – Burundi
95. Eddy Joassaint – Haïti
96. Efe Alexandra Omordia – Nigeria
97. Egyptian Front for Human Rights – Belgium
98. Eme Iniekung
99. Emeraude AMOUSSOU, Women Empowered – Benin
100. Emmanuel Acha – Nigeria
101. Emmanuel Pascal ZOHOUN – Benin
102. Equality Rights Africa Organisation (ERAO) – Namibia
103. Eric Ssali Abudallah – Uganda
104. Ese Emerhi
105. Evans Oduor, BAFOPE Youth Organization – Kenya
106. Faila KATALIKO – Democratic Republic of Congo
107. Family Harvest Foundation – Uganda
108. Fanny Fanou Ako, Women Empowered-Benin – Benin
109. Flora Lukudu Latio South – Sudan
110. Fountain of Hope (FOHOP) – Malawi
111. Friends of the Earth – Sierra Leone
112. From Heart To My Community Grace Foundation NGO – Zambia
113. Fundación De Derechos Humanos Karol Lizeth – Colombia
114. Fundación Frida Kahlo, Restaurando Vidas ONG – Colombia
115. Fundacion Kalu Ibaky – Panama
116. Fundacion Para el Desarrollo Integral Boliviano – Bolivia
117. Fundación Selva Sagrada – Ecuador
118. Fundación Váyalo – Venezuela
119. Gafidyn Rae Wesonga – Uganda

ORODHA YA WAUNDAJI -WENZA

120. Generation Activistes Capables (GAC) – Benin
121. Generation with A Mission-GWAM – Uganda
122. Giulia Bordin
123. Gladness Munuo – Tanzania
124. Global Participe – Republic of the Congo-Brazaville
125. Global Welfare Association (GLOWA) – Cameroon
126. Groupe de Recherche et d'Expertise en Développement Durable (GREDD-ONG) – Benin
127. Gunjan Veda – India
128. Gusoor for Peace & Coexistence – Yemen
129. Hafiz Jawad Sohail – Pakistan
130. Hands of Fortunate Passengers For Ethiopian Heroes (HFPFEH) – Ethiopia
131. Heather Luna
132. Hope For Vulnerable – Uganda
133. Humanitarian Enhancement Aid for Resilient Transformation-HEART – Bangladesh
134. Hussain Bux Korejo – Pakistan
135. IDTIDAMA Green Smart Cities NGO – Iraq
136. Inclusive Humanitarial Organization (IHO) – Ethiopia
137. Initiative for Right View (IRV) – Bangladesh
138. Initiative of Trans With a Mission - Uganda (ITWAM) – Uganda
139. Initiative pour la Promotion de la Santé Rurale et le Développement – Burundi
140. Innovazing Vision – Democratic Republic of the Congo
141. Institute for the Sustainable Development of Lenca Women of Honduras IDESMULH – Honduras
142. International Centre for Eritrean Refugees and Asylum Seekers – ICERAS and Arkobkobay – Sudan
143. International Helping For The Young – Chad
144. Isa kwambo Dagona – Nigeria
145. Isata Bridget Mansaray Kallon – Sierra Leone
146. Ismail Mire Foundation – Somalia
147. Isoke Kennedy BAGUMA – Kenya
148. Issa Hamad Alhewetat – Jordan
149. Janak Raj Hamal – Nepal
150. Jean Marie RUHANAMIRINDI – Democratic Republic of Congo
151. Jean-Daniel NDIKUMANA – Burundi
152. Jeremiah EBELEME – Nigeria
153. Jerome Dulin – Philippines
154. Job Sodalo – Togo
155. Joel K NGETICH – Kenya
156. Jones Shamalambo – Zambia
157. Joseph Obore
158. Jyoti M.Pathania

ORODHA YA WAUNDAJI -WENZA

159. Kalifani Lwanga – Uganda
160. Kalkal Human Rights Development Organization – Somalia
161. Karatu District Council – Tanzania
162. Kasimu Bello – Nigeria
163. Kelechukwu Okezie – Nigeria
164. Khmer National Liberation Front – Denmark
165. Kwizera Uwimana Josue – Rwanda
166. La Casa Grande – Benin
167. Landry BOUMBEYA – Congo
168. Lavenda – Kenya
169. Le Mont d'Or Sarl – Benin
170. Lizzy Nneka Igbine – Nigeria
171. Local Sustainable Communities Organisation Ltd (LOSCO) – Uganda
172. Lubaga Social Justice Center/Fellowship for Community Enlightenment – Uganda
173. LUBANGU Lumenge Jacques – Democratic Republic of the Congo
174. Lusoma Advisory
175. Lydia Odhiambo
176. M. Zakki Fuadi
177. Mahouna Guevara DAYOU – Benin
178. Maison Future Récolte – Democratic Republic of the Congo
179. Malango Maganga – Malawi
180. Manasseh Wepundi – Kenya
181. Mark Kebo Akparibo – Ghana
182. Marwa Eissa – Canada & Turkiye
183. Md Shariful Alam – Bangladesh
184. Medeto M. YETCHE – Benin
185. Men 4 Equality Trust – Zimbabwe
186. Might Foundation – Uganda
187. Moise Balagizi, DAI/ AU-ECOSOCC GA – Democratic Republic of the Congo
188. Mojisola Akinsanya
189. Motasem Zayed, Local Communities Organisation – Palestine
190. Mouvement Gabonais Pour la Promotion de la Bonne Gouvernance (MGPBG) – Gabon
191. Movement Against Food insecurity Organization (MAFO) – Sierra Leone
192. Mr. Festo Bali Christopher, South Sudan Community Change Agency (SOSUCCA) – South Sudan
193. Muhammad Zeeshan Farid – Pakistan
194. Multi Arts Alliance – South Africa
195. Multicultural Center Brusinka – Czech Republic
196. Nader Mahrous Louka Salama – Egypt
197. Nancy Mbaura – Zimbabwe
198. Nancy Wangai – Kenya

ORODHA YA WAUNDAJI -WENZA

199. Nasir Hassan
200. National Campaign for Sustainable Development Nepal – Nepal
201. National Movement For Emancipation and Progress – Sierra Leone
202. National Sudanese Women Association – Sudan
203. National Youth Action -NAYA, Inc. – Liberia
204. Nav Bhartiya Nari Vikas Samiti – India
205. NGAE Papin Gael – Cameroon
206. NGARASSAL Saham Jacques/Organisation Tchadienne Anti-Corruption – Chad
207. Nguzo Africa Community Foundation – Kenya
208. Nicholas Lee – Liberia
209. North Luzon Cinema Guild, Inc. – Philippines
210. OGC Enterprises – Tanzania
211. Ohaha Family Foundation – Nigeria
212. OIJPCR – India
213. Okello Michael – Uganda
214. Oladokoun Salomon BALOGOUN – Benin
215. Olawale F. Olaniyan – Gambia
216. ONG ADET – Togo
217. ONG PROBES – Benin
218. Paola Andrea Quiñonez, Fundación victimas Vulnerables Mujeres Afro Independientes(FUNVIMUFROIN) – Colombia
219. Papin Gael NGAE – Cameroon
220. Pathways for Women's Empowerment and Development (PaWED-IATC) – Cameroon
221. Paulina Nayra – Philippines
222. Pax Afrika Network (PAN) – South Africa
223. Peace for Women - West Nile – Uganda
224. Peace One Day Mali – Mali
225. People to Economic and Social Training – Jordan
226. PROMEDEHUM – Venezuela
227. RACI – Argentina
228. Randall Puljek-Shank
229. Reaccion Climatica – Bolivia
230. Recherche Sans Frontieres/RSF-RDC – Democratic Republic of the Congo
231. Red de Mujeres Hondureñas Contra la Violencia (REDMUHCV) – Honduras
232. Reem Gasim – Sudan
233. REPLALEZ – Peru
234. Reseau Jeunesse Service Guinée – Guinea
235. Resource Link Foundation Ghana (RLF) – Ghana
236. Ricardo Samaniego – Philippines
237. Ricky East African Foundation – Uganda
238. Rigoberto Lobo – Argentina
239. Rita Tchoupa Megnitio – Cameroon

ORODHA YA WAUNDAJI -WENZA

240. Rose MUCHANGA – Democratic Republic of the Congo
241. Rural Infrastructure & Human Resource Development Organization (RIHRDO) – Pakistan
242. Sadia Khan – South Africa
243. Salem Mohamed Ilyas – Morocco
244. Salwa Al-Zahid – Iraq
245. Samson AKON – Benin
246. Samudayik Sarathi – Nepal
247. Save The Lives Foundation – Pakistan
248. Service Anglican Pour le Développement Communautaire durable (SADC) – Burundi
249. Sessi Hypolite YOBODO – Benin
250. Sinatsisa Lubombo Women and Girls Empowerment Organization – Eswatini
251. Smile Orphanage Tanzania – Tanzania
252. Solidarité Pour l'Encadrement Et Lutte Contre La Pauvrete – Democratic Republic of the Congo
253. Sophie Kange – Uganda
254. Southern Africa Partnerships for the Prevention of Conflict (SAPPC) – Zimbabwe
255. Stanslous Chabala Mwansa – Zambia
256. Storm Shelter Initiatives Uganda – Uganda
257. Sugiarto Arif Santoso – Indonesia
258. Summit We Care For The Needy Foundation Kisumu – Kenya
259. Susan Njambi
260. Susan Wamalwa – Kenya
261. Sylvester Quee – Sierra Leone
262. Tahirou Bio Mamadou Yarou – Benin
263. Takaful Al Sham (TAS) – Turkiye & Syria
264. Tanzania Health and Education Organization(THEO) – Tanzania
265. Tanzania Youths Behavioral Change Organization (TAYOBECO) – Tanzania
266. The Emmanuel Ivorgba Center – Nigeria
267. The Hunger Project Zambia – Zambia
268. The Movement for Community-led Development Liberia / Interweaves Solutions – Liberia
269. The Tattaaunawa Roundtable Initiative (TRICentre) – Nigeria
270. Union des Jeunes Agriculteurs Modernes UJAM – Benin
271. Union pour la Promotion/Protection, la Défense des Droits Humains et de l'Environnement-UPDDHE/GL – Democratic Republic of the Congo
272. Ursul Amos BOUNDJA MANDAKOUZOU (Jeunesse Voie de la Paix) – Central African Republic
273. Uttanshi Agarwal – India
274. Vaï Valerie Yene Vai
275. Vemsat Youth Community Development Initiative – Nigeria

ORODHA YA WAUNDAJI -WENZA

276. Vision Globale d'Orientation des Jeunes – Democratic Republic of the Congo
277. Vision Haitienne des Droits de l'Homme VHDH – Haïti
278. Voices In the Vision for Africa (VIVA) – Zimbabwe
279. Volontaires Des Pays Des Grands Lacs – Democratic Republic of the Congo
280. Wallace Mawire – Zimbabwe
281. Watchman Relief Association Global – Cameroon
282. We Give Hope – Democratic Republic of the Congo
283. Welfare, Empowerment & Research Organization – Afghanistan
284. Women & Youths' Development Center Sierra Leone – Sierra Leone
285. Women Crusade for Development Africa – Uganda
286. Women Enablers Advocates & Volunteers for Empowering & Responsive Solutions (WEAVERS, Inc.) – Philippines
287. Women Relief Aid – South Sudan
288. Young Africans Community Empowerment Initiative, Sierra Leone (YACEI-SL) – Sierra Leone
289. Young Soul Uganda – Uganda
290. Youth Engaged For Development And Social Progress – Democratic Republic of the Congo
291. Youth for Peace & Dialogue Between Cultures – Morocco
292. Youth Partnership for Peace and Development – Sierra Leone
293. Youth Service Africa (YSA) – Benin
294. Youths Enterprise Development and Innovation Society (YEDIS) – Nigeria
295. Yusuf Ibn Tom

WASILIANA NASI

Movement for Community-Led Development
mcld.org
info@MCLD.org

CIVICUS
civicus.org
info@civicus.org

Peace Direct
peacedirect.org
info@peacedirect.org

MOVEMENT FOR COMMUNITY-LED DEVELOPMENT

CIVICUS

PEACE DIRECT